


# Matatizo ya kitaaluma na kimaadili katika vyombo vya Habari

MEDIA COUNCIL OF TANZANIA

# Matatizo ya kitaaluma na kimaadili katika vyombo vya Habari

Baraza la Habari Tanzania (MCT)
S. L. P.  10160, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 27757228 /2771947
Baruapepe: media@mct.or.tz
Tovuti: www.mct.or.tz

Matatizo ya kitaaluma na kimaadili katika vyombo vya Habari

©Baraza la Habari Tanzania, 2019

ISBN: 978-9987-710-73-7

Chapa ya Kwanza

# YALIYOMO


Utangulizi ........................................................................ 6

Misingi Mikuu ya Uandishi wa Habari......................... 8

Kutopendelea upande wowote: ...................................... 9

Ubinadamu: ..................................................................... 9

Uwajibikaji: ..................................................................... 10

Masuala ya Kimaadili ...................................................... 11

Kuandika Habari za Watoto: .......................................... 13

Kuwalinda Watoto:........................................................... 14

Kuomba radhi: ................................................................. 15

Kudhaniwa kuwa na hatia: ........................................... 17

Usisimuaji.......................................................................... 23

# Utangulizi

Ili kuwa na jamii imara yenye demokrasia na haki, kuwa na vyombo vya habari vya magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii ni muhimu sana. Lakini kwa vyombo vya habari kumweka kila mtu katika jamii- (hasa wale walio madarakani) akiwa anafuatiliwa mara kwa mara anachofanya, katika kuhakikisha kuwa demokrasia inazidi kuimarika na haki ina tawala, vyombo vya habari vinahitaji kujisimamia vyenyewe.

Nje ya vyombo vya habari, utaratibu huu umekuwa ukifikiriwa kwa muda mrefu kwa kuanzishwa kwa Baraza la Habari Tanzania (MCT). Hii ina maana kwamba vyombo vya habari havihitaji chombo kingine cha kuwasimamia mbali na hiki kilichopo hivi sasa. Chombo chao wenyewe huru na cha kitaaluma kinachoangalia kile wanachoandika kila siku.

Ina maana kuwa, kwa muda mrefu, jukumu hilo limekuwa ni kuimarishwa kwa vyombo vya habari kutoka ndani ya chombo chenyewe; hali hii imelazimisha kuwekwa mwongozo wa maadili iliyo rahisi kuzunguka nao kwenye vyumba vya habari; mwongozo ambao wale ambao ni wanataaluma ya habari na wasio wanataaluma wataweza kurejea wakati wanapoandika nakala zao au patokeapo mgogoro kuhusu namna ambavyo habari iliyochapishwa au kutangazwa ilivyoshughulikiwa.

Mwongozo wa maadili, ambao si mpya kwa waandishi wa habari, hufanyiwa marekebisho kila baada ya miaka mitatu. Umuhimu wa mwongozo huu upo kwenye ukweli kwamba, vyombo vya habari haviwezi kuchukua jukumu la kuwa mlinzi wa jamii iwapo vyenyewe havina mlinzi wake atakaye hakikisha kuwa waandishi wa habari wanafuata maadili ya taaluma yao kabla ya kuwanyooshea vidole wengine.

Pengine swali linalofaa zaidi hapa ni kwa nini hivi sasa? Jibu ni kwamba mwongozo huu unahitajika zaidi hivi sasa kuliko wakati mwingine wowote, kwa sababu, kwanza idadi ya vyombo vya habari na waandishi wa habari imeongezeka sana hivi karibuni.

Vile vile mwenendo mbaya wa kimaadili katika vyombo vya habari vya magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii nchini umekithiri sana na kusema kuwa, iwapo hakuna kitakachofanyika sasa na kwa haraka, tabia na mwenendo huo hautadhibitika tena.

Kinachotia wasiwasi zaidi ni kwamba makosa yanafanywa na kada ya waandishi wa habari ambayo imekwenda shule na ina wataalamu waliopata mafunzo zaidi ya watangulizi wao wa miaka ya 1970 ambao wengi wao walikuwa wamehitimu elimu ya sekondari tu.

Kuelewa uzito wa makosa haya ni muhimu kupitia, angalau kwa muhtasari, maadili ya msingi kwa waandishi wa habari, ni yapi, kwa kujiuliza swali lifuatalo: uandishi wa habari ni nini?

Mkurugenzi wa **Ethical Journalism Network,** Bw. Aidan White anasema: "Uandishi wa Habari ni kukusanya, kuripoti na kusambaza habari na taarifa kwa maslahi ya umma"

Anasema kuna takribani maadili ya kazi 400 duniani, yanayohusisha vipengele vyote vya uandishi wa habari, baadhi yake ni fupi na nyingine ni ndefu. Lakini yote yanazingatia maadili matano tu ya uandishi wa habari ambayo ni:

## Misingi Mikuu ya Uandishi wa Habari

**Usahihi:** Hii inahusu kutokuwapo na makosa. Katika msingi huu haitakiwi kushughulikia hoja kwa ujanja au udanganyifu. Waandishi wa habari wanafanya kazi zao kwa misingi ya hoja, habari inayozingatia au kutokana na hoja.

**Uhuru:** Msingi huu unamaanisha uko huru kutokana na udhibiti. Mwandishi hatakiwi kuingiliwa na mtu yeyote wakati anafanya kazi yake ya uandishi wa habari.

Kazi anayoifanya mwandishi wa habari ni yake; si kazi anayoifanya kwa niaba ya mtu mwingine yeyote.

Mwandishi wa habari siyo msemaji wa serikali wala wala hayupo chumba cha habari au sehemu yoyote anayofanyia kazi hiyo kwa ajili ya maslahi ya kikundi chochote cha biashara, kisiasa au kidini.

Anakuwa wazi kwa kila mtu unachofanya kwa hiyo anaposhughulika na hadhira, kutayarisha nyenzo kwa ajili ya vyombo vya habari vya magazeti au redio, televisheni na mitandao ya kijamii, anafanya kazi kwa uhuru kama mtaalamu.

## Kutopendelea upande wowote:

Msingi huu unamaanisha kutokuwa na upande kwa kila habari unayoiandika. Inahusu haja ya kutambua kuwa kuna zaidi ya upande mmoja wa habari, na bila ya shaka, mara nyingi, kuna zaidi ya pande mbili za habari. Kama mwandishi wa habari una jukumu la kuangalia na kufikiria je pande nyingine za habari ni zipi. Hiki ni kipengele muhimu sana kwenye kuandika habari.

## Ubinadamu:

Kama mwandishi habari unatakiwa kuonesha ubinadamu. Ni lazima uelewe matokeo ya kile unachopanga kuchapisha (kwenye gazeti) au kuhusu kile unachopanga kutangaza (kwenye redio, televisheni na mitandao ya kijamii). Ni lazima uelewe kuwa, wakati mwingine

maneno unayochapisha au picha unazoonyesha zinaweza kuharibu au kuwa na madhara kwa baadhi ya watu. Si jukumu la mwandishi wa habari kusababisha madhara kwa jamii. Ni kazi ya mwandishi wa habari kupunguza madhira kwa jamii.

Ni muhimu sana kujua kuwa wakati mwandishi wa habari anafanya kazi yake, hatakiwi kujihusisha na kauli za chuki, kuonyesha picha chafu au taswira ambazo zinadhihirisha wazi wazi bila ya sababu, ugomvi, machafuko, kwa sababu waandishi wa habari ni sehemu muhimu ya kuhakikisha kila kazi wanayoifanya wanatanguliza ubinadamu mbele.

## Uwajibikaji:

Hili pengine ni miongoni mwa mambo magumu sana kufanya kwa waandishi wa habari. Tunaona vigumu sana kusema bahati mbaya au samahani na kukiri makosa yetu, ingawa tunaweza kuwa wakosoaji wakubwa kwa wengine. Tunachoweza kufanya ni kushirikiana na hadhira na lazima tusahihishe makosa yetu na kutoa fidia tunapokosea". Aidan White anasisitiza.

Kwa hiyo kwa kupitia maadili ya vyombo vya habari, waandishi wa habari wanapaswa kuyafuata, mwandishi wa habari anakumbushwa mara kwa mara kile alichosem *White* hapo juu.

- **Vyanzo mbali mbali:**
  Chombo chochote cha habari ili kikubaliwe na wananchi inaotarajia kuwahudumia; habari na makala zake ni lazima ziwe na vyanzo mbalimbali. Vyanzo mbalimbali vinasaidia ukweli wa habari.

  Kwa mfano, utafiti uliofanywa na Baraza la Habari Tanzania (MCT), mara nyingi inaonyesha kuwa vyombo vya habari vya nchini vinakabiliwa na ugonjwa wa chanzo kimoja cha habari (SSS).

  Kilicho kibaya zaidi kuhusu SSS ni kwamba hutawaliwa na sauti za wanaume. Utafiti mmoja mahususi uliofanywa na MCT umeonesha kuwa gazeti la “Mwananchi” lilikuwa na habari 99 za SSS, habari za vyanzo viwili (63) na habari za vyanzo vingi (158), habari zenye sauti za wanaume 1,913 (95%) habari zenye sauti za wanawake 93 (5%).

  Utafiti huo huo pia unaonesha gazeti la “Nipashe” lilikuwa na habari za SSS 184, habari zenye vyanzo viwili (133), habari za vyanzo vingi (103), habari zenye sauti za wanaume 1,307 (94%) na zenye sauti za wanawake zilikuwa 88 (6%). Gazeti la “Uhuru” lilikuwa na habari za SSS habari zenye vyanzo viwili zilikuwa 155 na habari za vyanzo

vingi zilikuwa 204. Habari zenye sauti za wanaume zilikua 3,111 (95%) wakati sauti za wanawake zilikuwa 237 (8%). Takwimu hizo zinaonyesha ukubwa wa tatizo ambalo lazima lishughulikiwe haraka na vyombo vya habari vya ndani.

- **Picha mbaya**
  Hili ni tatizo ambalo vyombo vya habari, magazeti na redio, televisheni na mitandao ya kijamii ni lazima waliepuke. Picha mbaya haziimarishi jukumu kuu la vyombo vya habari, ambalo ni kuelimisha, kupasha habari na kuburudisha. Kinyume chake haziwapendezi wasomaji wa magazeti na watazamaji wa TV, kama ilivyo lugha chafu kwa wasikilizaji wa redio.

- **Haki ya kujibu:**
  Ni muhimu sana kwa chombo chochote cha habari kinachotaka kipewe umuhimu na wasomaji wake, wasikilizaji na watazamaji kuhakikisha kuwa kinafuata haki ya kujibu. Ni afadhali kuchelewesha habari mpaka anaye tuhumiwa apewe haki yake ya kujibu, kuliko kuitoa ikiwa na upande mmoja. Kutumia habari kwa sababu tu mtu hakupatikana kwa njia ya simu yake ya mkononi si utetezi dhidi ya haki ya mtu kujibu.

Ni vibaya zaidi iwapo mtu anatuhumiwa kukosea au ametajwa vibaya kwa namna moja au nyingine. Mfano

wa yaliyosemwa kwenye runinga ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Katika taarifa yake ya saa nne asubuhi iliyotangazwa na chaneli ya TV, Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru za 2018, Bw. Charles Kabeho, alioneshwa kwenye sehemu ya habari, akikataa kuweka jiwe la msingi katika jengo moja lililokamilika kujengwa Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro. Alisema amekataa kufanya hivyo kwa sababu mradi wa ujenzi wa jengo hilo ulikuwa na dalili zote za rushwa.

Mhandisi aliyehusika na mradi huo alijaribu kujieleza, lakini alinyamazishwa. Lakini chaneli hiyo ya TBC imeshindwa kuonyesha wazi wazi, picha ya mradi uliokamilika na hata kumpa nafasi mhandisi kuzungumzia suala hilo, na hivyo kuwanyima watazamaji fursa ya kutoa uamuzi wao wenyewe kuhusu tuhuma za Bw. Kabeho. Utafiti huo wa MCT umeonesha uadimikaji wa habari ambazo watuhumiwa walipewa haki ya kujibu.

## Kuandika Habari za Watoto:

Mapema mwaka 2018, wanawake waliolalamika kwamba wametelekezwa na wanaume wanaodaiwa kuzaa nao watoto, walifurika kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Hii ilikuwa baada ya ,Mkuu wa Mkoa kudai kwamba atawalazimisha kina baba “waliotoroka” kuwatunza “watoto wao” kwa siku kadhaa vyombo vya habari nchini – magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii vilionesha picha na sehemu ya wanawake, pamoja na watoto wao waliofuatana nao kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Hatua hiyo ya vyombo vya habari ni ukiukwaji

wa haki za maadili na sheria za watoto.

*The "Code of Ethics for Media Professionalism"* imeamuru vyombo vya habari kuwalinda watu wanaoishi katika mazingira hatarishi katika jamii na kuwa makini zaidi wakati wanaposhughulikia watoto. Katika mikutano yao, wanawake pia walimpa Mkuu wa Mkoa majina ya kina baba wanaotuhumiwa kuwa ndiyo wenye watoto hao wakiwemo viongozi wa chama, maofisa wa serikali na wanasiasa. Lakini wanaume wengi waliotajwa majina yao na vyombo vya habari, hawakupewa nafasi ya kujibu. Kwa kweli haikuwa halali!

## Kuwalinda Watoto:

Vyombo vya habari vinapaswa kuelewa mambo mawili kuhusu watoto. Kwanza, wengi wa watoto hao hawawezi kujieleza na kujua mahitaji yao, hasa ukizingatia umri wao ni mdogo, wanastahili ulinzi na haki zao za msingi kama walivyo watu wazima. Pili, na muhimu zaidi, ni ukweli kwamba watoto ni rahisi sana kudhuriwa, na kutokana na hali hiyo haki zao za binadamu zinaweza kuvunjwa kwa urahisi, kwa hiyo kuna haja ya vyombo vya habari kuwa mstari wa mbele katika kulinda haki za watoto hao wadogo. Kulinda haki za watoto wadogo maana yake sura zao zisioneshwe wakati haki zao za binadamu zinapokuwa zimevunjwa.

Mfano mzuri ni ule unaooneshwa kwenye habari iliyochapishwa katika ukurasa wa tatu wa gazeti la "Mwananchi" **Ukatili: Mtoto aingizwa kalamu sehemu**

**za siri.** Ingawa gazeti maarufu la kila siku la Kiswahili, limeficha jina la mtoto kwa usahihi kabisa, habari hiyo imetaja majina ya bibi yake, baba na jirani. Zaidi ya hayo, gazeti limetaja umri wa mtoto na mahali binti huyo anapoishi, na hivyo, kufanya kitendo cha kwanza cha muhimu cha kuficha jina la mtoto kisiwe na maana yeyote kwa sababu taarifa zilizotolewa kumuhusu mtoto huyo zimeandikwa kiasi kwamba watu wanaoishi jirani na mtoto huyo watamtambua kwa urahisi.

Kulinda utambulisho wa mwathiriwa, kwa upande mwingine wa watoto, maana yake ni kutoruhusu kutajwa watu au vitu vitakavyosababisha utambulisho wa mtoto huyo kujulikana. Hatua hiyo ya vyombo vya habari itampa mtoto huyo ulinzi kamili dhidi ya chuki wakati atakapo kuwa mtu mzima.

## Kuomba radhi:

Hii ni hatua inayohitaji kuchukuliwa haraka sana na chombo cha habari chochote mara tu kinapofanya kosa. Kosa hilo linaweza kuwa amefanyiwa mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu, taasisi ya umma au ya binafsi. Hata hivyo hali ya jumla inaonyesha kuwa vyombo vingi vya habari na hasa magazeti, havipendi kuomba radhi. Vinaelekea kufikiri kwa makosa kwamba kuomba radhi kutaathiri msimamo na hadhi yao machoni mwa umma. Lakini kinyume chake, kuomba radhi ni kuonyesha uaminifu na kukipatia chombo cha habari heshima kubwa kwa umma. Kwa matukio makubwa zaidi, kuomba radhi

kwa haraka kunaweza hata kukilinda chombo cha habari kisichukuliwe hatua ya kisheria.

Mfano mzuri wa kuomba radhi unaoneshwa na Gazeti la Nipashe la Juni 21, 2018. Gazeti hilo liliomba radhi kwenye ukurasa wa mbele baada ya kuchapisha habari kwenye ukurasa wa pili wa gazeti la Juni 20, 2018. Masahihisho na kuomba radhi vilitokea haraka katika toleo la Juni 21, 2018. Gazeti hilo la Kiswahili la kila siku liliandika habari yenye kichwa **"Upigaji Mabilioni Serikalini waibuka".**

Habari na kichwa cha habari vimebeba dhana kuwa ndani ya Serikali, kulikuwa na ufujaji au wizi wa mamilioni ya shilingi. Kwenye kuomba radhi mhariri alisikitika jinsi kichwa kilivyopotosha maana halisi waliyoikusudia na kuwaomba radhi wote waliokwazwa na habari hiyo.

Mfano mbaya wa kuomba radhi unaoneshwa na gazeti moja maarufu la Kiswahili ambapo gazeti lilifanya kosa mwezi Agosti 2010 na kuja kuomba radhi mwezi Novemba 2010. Hili kosa ambalo halitakiwa kufanywa na chombo chochote cha habari. Radhi inatakiwa kuomba kwenye toleo linalofuata baada ya kosa kugundulika limefanyika. Jambo moja ambalo linalokuwa kigezo kuwa habari hii ilikusudiwa kuwa ni kuomba radhi, ni tarehe ya kutolewa taarifa kwa vyombo vya habari, Agosti 2010, na kuchapishwa takribani miezi miwili baadaye, Novemba 16, 2010.

Badala ya kuonyesha wazi wazi kuwa taarifa hii ni kuomba radhi kwa kosa lililotokea kwenye toleo lililopita, mhariri ameamua kuficha kosa la gazeti lake kwa kuchapisha upya taarifa nzima iliyochapishwa katika toleo la mwezi uliopita bila ya kuwaarifu wasomaji wake sababu ya kufanya hivyo.

Hata hivyo ukipitia habari hiyo, msimamo na maudhui umeonesha kuwa gazeti hilo lilikuwa likiomba radhi kusiko moja kwa moja kutokana na habari isiyo sahihi iliyochapishwa zamani.

## Kudhaniwa kuwa na hatia:

Kikatiba, mtu hadhaniwi kuwa na hatia mpaka ithibitishwe na mahakama. Hili ni sharti la lazima la kikatiba ambalo ni lazima liheshimiwe na vyombo vya habari. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha mara nyingi vyombo vya habari nchini **"vinajaribu na kuwatia hatiani watuhumiwa"** hata kabla ya kufikishwa mahakamani. Mfano mmoja wa habari ya mahakamani iliyokuwa na upungufu mkubwa iliripotiwa Agosti 9, 2018 kwenye ukurasa wa 24 wa gazeti la "Uhuru" yenye kichwa cha habari kinachosomeka **"Apandishwa Mahakamani kwa Ubakaji".**

Kichwa hicho cha habari kinaonesha kuwa mtuhumiwa tayari amepatikana na hatia ya kubaka. Hata hivyo wakati habari ilipochapishwa, mahakama ilikuwa bado iko kwenye mchakato wa kusikilizwa na bado ilikuwa

haijabainika hatia au vinginevyo ya mshitakiwa.

Kwa hiyo ingekuwa bora zaidi kuandika kichwa cha habari kitakachoonesha hali ya kesi ilipofikia, maana yake mtu huyo bado hana hatia na atabaki hivyo mpaka itakapo thibitishwa na mahakama.

Gazeti la Nipashe la Julai 28, 2018, lilichapisha kichwa cha habari cha kuhukumu kwa ajili ya habari yake mpaka kwenye ukurasa wa 9, iliyosomeka: **"Polisi yanasa watu 40 kwa uhalifu".**

Ni muhimu kuzingatia kuwa hao watu 40 ni watuhumiwa tu, kwa wakati huo hawakuwa wahalifu na wajibu wa kuthibitisha iwapo wameshiriki au hawakushiriki kwenye uhalifu upo mikononi mwa mlalamikaji ambaye ni lazima airidhishe mahakama kubaini iwapo mshitakiwa ana hatia au la.

Ndiyo maana, mara mtu anapokamatwa na polisi, mtuhumiwa ni lazima afikishwe mahakamani ndani ya muda wa saa 24.

Hata hivyo wahariri, wana tabia za kuandika vichwa vya habari vinavyotoa hukumu ili kuwavutia wasomaji wanunue magazeti yao. Lakini mtu mwelewa anapoachiwa huru na mahakama baada ya kubainika kuwa hana hatia, anaweza kuamua kufungua kesi dhidi ya gazeti

lililoandika au kutoa picha kuwa ni sehemu ya kundi la wahalifu ambalo polisi imedai kuwa ni genge la wahalifu. Bila shaka gazeti linalohusika huenda likakabiliwa na mkono wa sheria.

Kwa muhtasari, kutumia picha za watu ambazo polisi wanadai ni wahalifu, au utoaji wa matamko kuhusiana na tukio hilo, havitamzuia mhariri kushitakiwa kwa madhara aliyoyasababisha kwa watuhumiwa iwapo wataachiwa huru na mahakama.

- **Maelezo ya polisi kuhusu uhalifu au kifo si ya mwisho:-**
  Imekuwa ni jambo la kawaida kwa vyombo vya habari nchini kupokea maelezo ya polisi kama ni ya kweli na ya mwisho kabisa. Si kweli! Watu wanaokamatwa na polisi kwa kutuhumiwa kuwa wamehusika katika uhalifu ni lazima vyombo vya habari vione kuwa ni zaidi ya kukamatwa kwa nguvu kwa watuhumiwa tu. Hali hiyo ni sawa na madai ya polisi kuwa idadi kadhaa ya watu wanasemekana kufariki dunia, katika labda, ajali ya barabarani. Itokeapo ajali ya aina hiyo, au ajali yeyote, ni wajibu wa mwandishi kumuuliza polisi anayetoa taarifa hiyo kama je daktari amethibitisha kifo cha mtu au watu?

- Pia imekuwa ni jambo la kawaida polisi kuwapanga

watu waliokamatwa mbele ya vyombo vya habari. Wakati mwingine watu hao wanapangwa pamoja na silaha zinazosemekana walikuwa nazo wakati wa kukamatwa kwao.

Mara nyingi polisi wanaodai kuwakamata watu hao ama walikuwa wanakaribia kufanya uhalifu au wakiwa wanafanya uhalifu. Magazeti au vituo vya televisheni vimekuwa vikiendelea kuchapisha au kuwapanga watu hao. Vyombo vya habari nchini vimekuwa na bahati kwamba watu hao ambao mwishoni huachiwa huru kwa kukosekana ushahidi, hawajawahi kurudi tena mahakamani kudai fidia kwa "kutiwa hatiani" na vyombo vya habari kwa makosa ya uhalifu ambayo hawakufanya.

Hata hivyo, kadiri matukio ya namna hiyo yanavyoendelea, Watanzania wataamka na kuelewa haki zao kuhusiana na baadhi ya vyombo vya habari kuwahukumu kabla ya mahakama kutoa uamuzi na vitaishia kujutia walichokifanya.

- **Matumizi ya maneno ya kibaguzi au ya kukashifu:** Kama ilivyoelezwa kwenye utangulizi wa "Mwongozo wa Maadili ya Vyombo vya Habari" jukumu la vyombo vya habari katika jamii ni kuchapisha habari, kuelimisha na kuburudisha.

- Hata hivyo vyombo vya habari haviwezi kufanikiwa katika kupasha habari au kuwaelimisha watu katika jamii inakofanya shughuli zake, iwapo inatumia maeneo ya kibaguzi na ya kukashifu.

- Waandishi wa habari wanatakiwa kuwa waangalifu kwa haki na utu wa watu wote bila ya kujali rangi, jinsia, kabila, umri , ulemavu, jiografia au jamii.

Mifano ya habari ambazo hazikuzingatia matumizi ya maneno hayo ya kibaguzi ilitolewa na gazeti la Nipashe la Juni 30, 2018, ukurasa wa tatu wa gazeti hilo.

Nipashe liliandika habari yenye kichwa cha habari: **"Kikongwe akatisha uhai kwa kujikata mshipa na kisu".** Kwa kiswahili neno "Kikongwe" linashusha heshima, maana yake linahusu mzee sana, hasa mwenye makunyazi kutokana na umri. Badala ya kutumia neno linaloshusha heshima licha ya kuwa mzee, neno la kiungwana ni "Mzee" lenye maana ya mtu mwenye umri mkubwa lingefaa. Hakukuwa na haja ya kutoa maelezo ya kina jinsi mtu alivyojiua.

Katika gazeti hilo hilo la Agosti 7, 2018 katika ukurasa wa tatu, lilichapisha habari yenye

kichwa cha habari **"Lugola aonya kampuni za ulinzi kuajiri vikongwe".** Lugola anayetajwa hapa ni Waziri wa Mambo ya Ndani wa sasa (2019), Bw. Kangi Lugola. Neno "vikongwe" ni wingi ya "kikongwe", neno ambalo tumelifafanua na kulikosoa hapo juu. Hatukuambiwa kwanini Waziri hataki wazee waajiriwe na kampuni za ulinzi, ingawa tumeona kichwa cha habari kikisema hivyo. Lakini si vigumu kukisia kwa nini, kwa sababu ya ukweli kwamba wazee si chaguo bora kwa kazi ya ulinzi kwa sababu watakosa uwezo na nguvu ya kupambana na wahalifu.

- Julai 16, 2018 katika ukurasa wa 10 wa gazeti la Nipashe lilichapisha habari yenye kichwa cha habari, **"Serikali yakumbuka wanafunzi viziwi".** Neno "kiziwi" (umoja wa viziwi) yenye maana mtu mwenye ulemavu wa kusikia, lilikuwa linatumiwa zamani, lakini kwa utamaduni wa sasa linasemekana kuwa si la uadilifu au lisilo na staha. Badala ya kutumia neno "viziwi", kichwa cha habari kingesomeka, **"wenye ulemavu wa kusikia"**

- Neno jingine la kushushia heshima kwenye kichwa cha habari kile kile ni **"yakumbuka"**. Jinsi neno **"yakumbuka"** lilivyotumiwa kwenye kichwa cha habari pia ni la kushushia heshima,

kwamba Serikali mpaka sasa imewasahau watu wenye ulemavu wa kusikia. Kichwa cha habari sahihi kingekuwa; **"Serikali kuboresha hali ya wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia".**

## Usisimuaji.

Huu ni ustadi unaotumiwa na baadhi ya wahariri, hasa kwenye magazeti, ili kuongeza mauzo ya magazeti yao. Mfano mzuri wa habari yenye usisimuaji umo kwenye "Ripoti ya Ufuatiliaji ya MCT" iliyohusisha vyombo vya habari vya nchini kati ya Julai 2010 na Juni, 2011.
Ripoti ya MCT inatoa mfano wa habari iliyoandikwa kwenye gazeti moja la Kiswahili la Novemba 2, 2010. Gazeti linalohusika liliandika habari yenye kichwa cha habari, **"Akamatwa kwa kufanya mapenzi na mbwa Morogoro".**

Habari hiyo ilitaja chanzo kuwa ni Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro ambaye alinukuliwa zaidi kwenye habari hiyo akisema mbwa huyo baadaye alibainika kuwa mjamzito na kwamba mtuhumiwa aliyekamatwa inasemekana ndiye aliye husika na ujauzito huo.
Iwapo mhariri angekuwa mtaalamu kwenye kazi yake, asingeruhusu kuchapishwa kwa habari hiyo bila ya kuhakikisha kuwa kama inawezeka binadamu kufanya ngono na mbwa, pia iwapo kisayansi inawezekana

binadamu kumpa mbwa mimba.

Ili kupata majibu sahihi, mhariri lazima angewasiliana na madaktari wa binadamu na wa mifugo.

Kutokana na mhariri kutochukua hatua yeyote kati ya zilizotajwa hapo juu kuhakikisha ukweli wa habari hiyo kwa uwazi, inaonesha kuwa lengo lake lilikuwa kusisimua habari ili kuongeza mauzo ya gazeti lake.

Hata kama si mtaalamu, kueleza kitendo cha mwanaume kufanya ngono na mnyama (Kitendo cha kinyama) kuwa ni "kufanya mapenzi" ni ishara ya dharau.

Kwa miaka kadhaa sasa, wahariri wamekuwa wakifahamika kutoa vichwa vya habari vya kusisimua ambavyo havioneshi maudhui ya habari. Vichwa vya habari vya aina hiyo, vinatumiwa kukuza mauzo ya gazeti.

Tabia ya kutumia vichwa vya habari vya aina hiyo inaonekana kwenye magazeti makuu na magazeti ya udaku. Lengo, kama ambavyo imeelezwa hapo awali ni kuwavutia wasomaji.

Hali hii pia inachangiwa na kuingia kwenye tasnia ya habari kizazi kipya cha waandishi wa habari, ambacho licha ya kuwa na utaalamu, elimu bora, bahati mbaya ni wavivu na hivyo kutegemea habari zao kutoka kwenye

mikutano na vyombo vya habari, warsha, semina na taarifa kwa vyombo vya habari.

Tatizo linakuwa ngumu zaidi kwa kutumia waandishi wa gharama nafuu katika vyombo vya habari. Hatua hiyo haijasaidia kutokana na baadhi ya vyombo vya habari kushindwa kulipa mishahara yao ya uandishi wa habari kwa hadi miezi mitano.

- **Propaganda**

  Hii ni taarifa ya upande mmoja au inayopotosha, inavyotumika kuhimiza mwelekeo wa kisiasa au hoja fulani ya maoni. Wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, mojawapo ya gazeti la Kiswahili la kila siku la "Uhuru" liliandika habari kwamba Chadema imewapeleka zaidi ya vijana 1,000 kwenda Rwanda kwa mafunzo ya kijeshi kwa ajili ya kujiandaa kufanya fujo wakati wa uchaguzi.

- Hata hivyo gazeti hili halikufanya utafiti wowote wa habari hiyo waliyoichapisha na wala hawakunukuu au kumtaja mtu yeyote, vyanzo vyovyote ambavyo vimeipa uzito habari yao.

- Kilichokuwa kinawafurahisha zaidi ni kwamba, licha ya athari kwa usalama wa taifa, haikuelezwa kuwa wakuu wa vyombo vya usalama vya nchi

wamekwenda kuhoji mhariri wa gazeti kuhusu vyanzo vya mwandishi.

Lakini hali ya kuwa habari ilichapishwa wakati wa kampeni za uchaguzi, haikuwa vigumu kuihusisha na jaribio la kutaka kupaka matope Upinzani.

- **Uraghibishaji wa Vyombo vya Habari kwa Manufaa ya Taifa**

  Licha ya jukumu lake muhimu la kupasha habari, kuelimisha na kuburudisha jamii, vyombo vya habari visitekeleze jukumu la uraghibishaji, hasa kwa manufaa ya taifa yanayojumuisha pia mambo mengine, mapambano dhidi ya ukiukaji wa uhuru wa vyombo vya habari na haki za binadamu.

- Mfano mmoja mzuri wa ushiriki wa vyombo vya habari katika kupambana kwa manufaa ya taifa ni jinsi ya kushughulikia kupotea kwa watu nchini wakati mwandishi wa habari wa gazeti la Mwananchi Azory Gwanda, alipopotea mwaka mmoja uliopita, ni magazeti machache tu ndiyo yaliyochapisha picha yake na kuuliza maswali.

- Licha ya machapisho ya vyombo vya habari vya Mwananchi Communications Limited, vyombo vya habari vingine havikuonesha kujali nini kilichotokea.